

Pampu ya zege (PeP) Concrete Pedal Pump

PeP ilitengenezwa na wahandisi wa Uswiss. Hivi sasa inatengenezwa na kutumika katika nchi zaidi ya kumi.

Chama kiliundwa ambacho kiliitwa **W₃W** (Water for the Third World) kinachojishughulisha na matatizo ya maji katika nchi zinazoendelea.



Hadi kufikia leo zaidi ya pampu 3500 zimetengenezwa na zinatumika katika nchi mbali mbali za ulimwengu. kama India, Kenya, Tanzania Uganda, Peru, Burkina Faso, Msumbiji na Madagascar.



W₃W iliweka malengo na ilifanikiwa kuyatimiza kwa msaada wa wakulima wengi kutoka nchi mbalimbali za ulimwengu pamoja na mawazo mapya kutoka kwa wataalamu wa Uswiss. Malengo hayo yalikuwa ni:

- Pampu inayoweza kutengenezwa kirahisi katika karakana ndogo za vijijini.
- Pampu inayoweza kutengenezwa kwa kutumia malighafi na vifaa vinavyopatikana kwa urahisi hapa nchini.
- Pampu inayoweza kukarabatiwa na mkulima mwenyewe kwa gharama ndogo.

Uwezo wa pampu ya zege (PeP)

Pampu hii ina uwezo wa kumwagilia bustani na mashamba na kumpatia mkulima mavuno mazuri na hivyo kumwongezea kipato. Pampu inaweza kutosheleza bustani za ukubwa kama ifuatavyo:

- Mboga, kama nyanya, vitunguu, bilinganya, nyanya chungu, bamia, **ekari moja**
- Vitalu vya miti ya matunda. **nusu ekari**



Sifa za pampu ya zege PeP – Concrete Pedal Pump:


- Imetengenezwa kwa teknolojia rahisi na ya kufaa.
- Huendeswa kwa miguu, ni nyepesi na rahisi kuendeshwa.
- Inaweza kutengenezwa na kukarabatiwa katika karakana za vijijini
- Ina uwezo wa kuvuta maji hadi lita 100 kwa dakika.
- Pampu hii inaweza kuvuta maji hadi kina cha mita 6 mpaka mita 8 juu, na katika tambarare umbali wa mita 200.
- Haitumii mafuta wala umeme na inadumu muda mrefu.
- Haishiki kutu kwa sababu imetengenezwa kwa zege pamoja na PVC.
- Gharama ya kukarabati ni ndogo sana.

Kutokana na sifa zilizotajwa hapo juu mkulima ataweza kufanikiwa, na kupata mavuno mengi kwa kutumia pampu ya zege (CPP).

KARIBU UJIPATIE PAMPU YAKO:



Kwa taarifa zaidi wasiliana na:



W≈3≈W
Ofisi Kuu
iliyopo
Tushikamane VTC
P.O.Box 765
Morogoro Tanzania

Tel:
+255 (0)732 - 931 031
+255 (0)23 - 2600 481
Email:
tanzania@w-3-w.ch
w3w_tz@hotmail.com

Mr. Yanga Mwangindo, Director
Cell: +255 (0)754 - 443 932

Mr. Ezekiel Mpogole, Chief Technician
Cell: +255 (0)713 - 081 337

Mafundi wetu:

Jina:

Mahali:

Anuani na Simu:

W ≈ 3 ≈ W

inawaleteta

Pampu ya Zege C P P

(Concrete Pedal Pump)

www.w-3-w.ch

Ufumbuzi wa umwagiliaji wa bustani za mboga, mashamba na matumizi ya nyumbani.



W≈3≈W

Water for the Third World - Association

P.O.Box 765, Morogoro, Tanzania
Tel: +255 - (0)23 - 2600481
+255 - (0)732 - 931 031